Teacher.co.ke

**KISWAHILI KIDATO CHA TATU**
**MUHULA WA KWANZA 2023**
**MUDA: SAA 1**
**Jibu maswali yote kwenye nafasi ulizoachiwa wazi baada ya kila swali.**

**SEHEMU YA A: UFAHAMU (ALAMA 15)**
**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuatia.**

Mtopanga ni miongoni mwa vitongoji vinavyopatikana katika nyanda za janibu yetu. Kitongoji hiki kina sifa zilizosambaa karibu na mbali, na kukifanya kutukuka sana. Asili ya utukufu wake ni mandhari yake, labda jambo hili ndilo raghba ya hapa. Maskani haya yana majumba ya watu wa matabaka yote. Kuna makazi ya madongoporomoka na vile vile majumba ya wakwasi. Ajabu ya kitongoji hiki ni ile ya kutokuwepo kwa mipaka baina ya wachochole na wale walioinukia kiuchumi, na kama ilitokea ilikuwa ni nadra sana. Mapaa ya majumba yao yanashikana kama safu ya meno ya msumeno. Unawajibika kuinama unapopita katika kijiji hiki. Walioinuka kiuchumi hujizatiti kwa vyovyote kuwasaidia na kukirimu wale wengine ili maisha yao nao yapate ahueni. Hili limefanya hali ya maisha yawe rahisi na kustahimilika na kila mahuluki.

Maskani ya watu wa nchi yamejengwa vizuri lakini yameinama chini na kusongamana kama safu ya milima ya Everest. Jambo hili limezusha jina la lakabu "vibyongo?". Lakini lingine linalowakumba wanakitongoji hawa ni maradhi.

Dhiki ya maradhi inashughulikiwa na wataalamu walio mahiri na kutaalamika katika taaluma mbalimbali za uganguzi. Ushindi wao unategemea juhudi za wataalamu hawa. Ujinga ni jambo lililo gumu kuondoa na kila mwanakijiji analishughulikia jambo hili. Kisomo cha watu wazima huendelezwa ili kuwaelimisha wote juu ya mpango wa kusoma.

Kitongoji hiki kina ziwa kuu kwa upande wa machweo. Ziwa hili hutoa mvuke ulio fufutende ambao hufanya mavundevunde. Mto Hari ulio katika kitongoji hiki humwaga maji yake hapa. Mto huu hauna samaki na maji yake hutokota kwa kipimo kikubwa cha joto. Wenyeji wa hapa aghalabu hutumia maji ya mto huu kupikia viazi, mayai na hata kuchemsha samaki. Labda huu ndio mto unaoongezea mastakimu haya umaarufu wake. Mto mwingine ulio hapa ni Mto Salama, ambao hupita kando ya ziwa hili.

Mto huu hutoa maji yaliyo baridi sana. Wanakitongoji huyachukulia maji haya kama mafuta ya tunu. Hali kadhalika huamini kwamba mtu yeyote anayejisinga kwa maji ya mto huu, ngozi yake hung'ara kama theluji. Mbali na manufaa hayo yote, si rahisi kuogelea au kuvuka mto huu kwa usalama. Wakazi wa hapa hungoja wakati mto huu umekauka na kwenda kujisinga katika vidimbwi vya maji yaliyosalia.

Mashariki mwa kitongoji hiki ni sehemu iliyotengwa mahsusi kwa pareto, mawele, wimbi na mtama. Katika kupalilia wao hutumia viserema. Kulima sesa ni jambo lisiloachwa nyuma. Miti ya kijiji hiki ilipandwa kwa miche hamsa wa mia na imeendelea kunawiri na kukua zaidi mithiri ya makonde yaliyonyunyiziwa marashi ya miwaridi. Ukipita hapa utafikiri unaambiwa 'shikamoo'. Matawi ya miti hii inanong'onezana na ardhi iliyo vuguvugu kwa unyevu wa matawi yanayotoa chemchemi za maji kutoka ardhini ili kurashia hewa inayozizima na kufanya mahali hapa jambo la shani. Wao huona kuwa haya ni maumbile ya kawaida

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

yasiyohitaji kuajabiwa.  Miti mingi huwa na kimo cha chini ya mita tano.  Nyanda za chini za kijiji hiki, miti yenye kimo cha mita mbili hupatikana na mibirimbi hukua hadi kimo mkono wa tembo.  Hata hivyo ni nadra sana kuipata miti hii ambayo matunda yake hutumiwa sana na wenyeji kama kiungo cha mchuzi.

Njia za miguuu zimejengwa kwa mawe yaliyotoka katika milima ya volcano na kusakafiwa kwa saruji.  Barabara za magari ni pana na si rahisi kwa magari kusababisha ajali.  Huduma za usafiri zimeimarika katika kijiji hiki.

**MASWALI:**

(a) Taja sifa tatu za kijiji hiki (alama 3)

(i) Makaazi ya watu wa matabaka yote
(ii) Nyumba za aushi
(iii) Nyumba za muda-udongo huporomoka
(iv) Ziwa kuu litoalo mvuke fufutende
(v) Mto Hari wenye maji moto sana
(vi) Mto Salama wenye maji baridi sana

(b) Eleza vile watu wa kijiji hiki cha Mtopanga wanavyojaribu kusawazisha hali yao ya maisha. (alama 3)

(i) Kiuchumi: Walionavyo huwasaidia wachochole
(ii) Kielimu: Wopte wanashiriki kuongozana
(iii) Kiafya: Wana wataalamu wa taaluma mablimbali za uganguzi.

(c) Mto salama huwasaidiaje wenyeji wa hapa. (alama 2)

Wenyeji huyatumia maji yake kuwa dawa

(d) Eleza maana ya vifungu hivi vya maneno. (alama 4)

(i) Miti inasema “Shikamoo” – hali ya miti kuvutia kwa rangi na kivuli

(ii) Kunong’onezana na ardhi – kunawiri na kukua hadi kuinamia ardhini

(iii) Hamsa wa mia – mia moja na tano

(e) Eleza maana ya msamiati huu kama ulivyotumiwa katika kifungu. (alama 3)

(a) Janibu – Pande/sehemu

(b) Mahuluki – watu/wanadamu

(c) Mastakimu – makazi/maskani

**SEHEMU YA B: MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

1. (a) Taja vigezo vitatu vya kuainisha irabu za Kiswahili. (alama 3)

(i) Sehemu ya ulimi inayotumiwa kutamka
(ii) Mwinuko wa ulimi
(iii) Hali ya mdomo

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

(b) Andika sauti zenye sifa zifuatazo: (alama 2)

(i) Kipasuo ghuna cha midomoni /b/

(ii) Nazali ya ufizi /n/

2. (a) Tofautisha kati ya silabi funge na wazi, huku ukitolea mfano mmoja mmoja. (alama 2)

(i) Silabi funge huishia Konsonanti k.v. Dakatri, Maktaba n.k.
(ii)Silabi wazi huishia kwa irabu, k.v kitabu, kisu, maziwa n.k.

(b) Andika neno lenye muundo ufuatao: (alama 2)
Nafsi ya tatu, wakati uliopita, mzizi, kiishio.
Wa-li-som-a au Walisoma.

3. (a) Bainisha vielezi katika sentensi ifuatayo. (alama 3)
Watoto wale walipochezea barabarani waliadhibiwa baadaye
Po-kielezi cha wakati
Barabarani – kielezi cha mahali
Baadaye – Kielezi cha wakati

(b) Onyesha taofauti katika sentensi hizi (alama 2)
Ningalikuwa mwalimu ningalishiriki mgomo
Ningekuwa mwalimu ningeshiriki mgomo
- Ngali – Matumaini ya kitendo kutendeka hamna
- Nge - Matumaini ya kitendo kutendeka yapo au kuna uwezekano

4. (a) Onyesha matumizi ya ni katika sentensi hii.
Niliyemsaidia ni huyu lakini sasa simameni muende uwanjani.
Niliyemsaidia – Nafsi ya kwanza umoja
ni – Kitenzi kishirikishi kipungufu
Simameni – Wingi hali ya kuamrisha

(b) Andika usemi wa taarifa. (alama 3)
“Maria! Maria! Njoo hapa,” mama akamwita. Kesho nitaenda Nairobi, kesho kutwa Kisumu na sasa ninaenda huko sokoni”
Mama alimwita Maria mara mbili kwa kumwambia aende hapo alipkuwa na kumwezeza kuwa siku ambayo ingefuata angeenda Nairobi, siku ambayo ingefuata hiyo Kisumu na saa hiyo akuwa akienda kule sokoni.

5. (a) Kanusha. (alama 2)
Alilia na kulaani.
Hakulia wala kulaani

(b) Tunga sentensi mbili tofauti kuonyesha matumizi ya vitenzi vifuatavyo katika hali ya kutendwa. (alama 2)
Cha
(i) Mungu anachiwa na kila mja

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

Oa
(ii) Msichana yule ataozwa kwa kijana huyo kesho

6. (a) Badilisha kitenzi kilichopigiwa mstari kiwe kivumishi. (alama 2)
Alioga kwa maji baridi
Fisi mwoga aliuwawa na Simba.

(b) Eleza maana ya mzizi wa neno huku ukionyesha mzizi katika vitenzi fivuatavyo. (alama 4)
**Mzizi: Sehemu ya kitenzi ambayo haibadiliki kamwe wakati wa mnyambuliko.**

(ii) Watakuja
**Mzizi ni –j-**

(iii) Wataandika
**Mzizi ni –andik-**

7. (a) Onyesha taofauti kati ya sentensi hizi (alama 2)
Kuku yeyote atachinjwa **(bila kubagua)**
Sukari yote itauzwa (**kwa ujumla)**

(b) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa (alama 3)
Nguo ambazo zinauzwa kwenye duka hilo zinavutia.
**Maguo ambayo yanauzwa kwenye jiduka hilo yanavutia**

8. (a) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao. (alama 2)
U + T + E + T + N
**Ili apite vizuri, atasomea mtihani**

(b) Huku ukitolea mfano katika sentensi, onyesha kiwakiloishi nafsi huru na nafsi ngeli. (alama 2)

**(i) Mimi nitajitahidi masomoni (Nafsi)**
**(ii) Atafikishwa mahakamni Leo**

**SEHEMU YA C: ISIMU JAMII (ALAMA 15)**

**9. "Bwana mdogo," alisema kwa sauti ya kite.**
"Naam, Doctor," nikajibu
"Leo wasikiaji?"
"Nafeel poa"

**(a) Tambua sajili. Thibitisha. (alama 3)**

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

(i) Sajili ya hospitali
(ii) Ithibati: Doctor, nafeel.

**(b) Eleza sifa sita zinazojibainisha katika sajili husika. (alama 12)**

- Kuna matumizi ya lugha mseto kama vile – Naam Doctor
- Lucha ya heshima – bwana mdogo
- Lugha wazi – Leo nasikia vizuri
- Sentensi fupifupi – Nafeel poa
- Msamiati teule wa hospitali – Doctor
- Mgonjwa kuulizwa maswali – "Leo wasikiaje?"

**SEHEMU YA D: TAMTHILIA**

**PAULINE KEA: KIGOGO (ALAMA 20)**

**Thibitisha kwa kina ufaafu wa anwani Kigogo (alama 20)**

- Kigogo ni mtu mwenye madaraka makubwa ya kiutawala. Ni mtu mkubwa mwenye madaraka. Ni mtu mwenye nguvu za kutawala. Tamthilia ya Kigogo imejengeka kwa kumzunguka mhusika ambaye ndiye Kigogo wa Sagamoyo, mtawala mwenye nguvu na mamlaka ya kutenda apendavyo.

- Majoka ni mwenyte nguvu za kuangamiza wapinzani wake kama vile Jabali na chama chake cha mwenge. Tunu aliponea chupuchupu. Alikuwa auawe badala yake akavunjwa miguu.

- Isitoshe anapogundua kuwa mambo yamezidi unga, anamwamuru Kingi kuwapiga risasi. Anaosema wapigwe risasi ni watu waliokubali wito wa Tunu kukusanyika mbele ya lango kuu la soko la Chapakazi.

- Majoka ni Kigogo kweli, mtu mwenye nguvu. Boza anamwonya Sudi dhidi ya kubishana na mwenye nguvu. Sudi alikataa kuchanga kinyago cha ngao kama alivyoulizwa na Kinga. Alibishana na Kinga. Boza akamshauri kuwa udongo haubishani na mfinyanzi. "Kigogo hachezewi, watafuta maangamizi.

- Mazungumzo baina ya Majoka na Ashua yanadhihirisha Majoka ni mwenye nguvu, ni Kigogo na hapendi ubioshani. Ashua anapomwambia ukweli kuwa mtu katika Sagamoyo hawezi kupata haki maana Kipanga ndiye hakimu kwa kuku, Majoka anamwonya, "Wasema na Kigogo wa Sagamoyo kumbuka"

- Nguvu za Majoka zinadhirika pia kiuchumi. Aliamuru soko la Chapakazi lifungwe na likafungwa nao wafuasi wake vipofu kama Ngurumo na Boza wanafurahia jambo hilo maana watu walipokosa la kufanya wengi walikimbilia ulevini.

- Nguvu za Kigogo huyu zinadhirihika wakatu watu walikataa kuhudhuria sherehe za uhuru katika ikulu ya Majoka, wakaenda kumsikiliza "Kigogo" mpya mbele ya lango la soko la Chapakazi. Tunu ni Kigogo si kwa njia ya uchaguzi bali kwa nguvu alizopewa na umma unaomwamini, kwamba anaweza kuleta mabadiliko katika jimbo la Sagamoyo.

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

- Kigogo wa jimbo hili la Sagamoyo ni mwenye nguvu za kutenda maovu na kuyaficha. Kwa mfano ajali iliyomuua Jabali lilangwa nay eye na watu wake wakafurahia kuwa raia hawakujua hivyo.

- Majoka ni Kigogo kweli. Ana nguvu za kuvunja sheria za katiba. Kwa mfano mamapima, alipata kibali cha kuuza pombe haramu kutoka kwa serikali ya Majoka licha ya kuwa kinyume cha sheria.

- Nguvu za Majoka zinadhihirika kwa namna alivyo na wafuasi sugu kama vile Boza, Kinga, Ngurumo na wananchi wengidd kwa jumla. Aliamini hangepata upinzani. Anamwambia Kenga "Watu wa Sagamoyo ni wangu, hawawezi kuwa wa Tunu"

- Kingi pia ni mwenye nguvu. Ni Kigogo. Ni mkuu wa polisi mwenye nguvu za kuwatawanya waandamanaji wanaompinga majoka. Tunu anakiri kuwa Kingi alikuwa amekubali kuwalinda badala ya kuwatawanya kama alivyofanya awali kwa wiki kadhaa.

**<u>SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI (ALAMA 10)</u>**

**1. (a) Eleza maana ya Ulumbi.** **(alama 2)**

Huu ni uhodari wa kutumia lugha kwa ufundi wa kipekee

**(b) Fafanua sifa zozote nne za Ulumbi.** **(alama 8)**

- Ulumbi ni usemaji au uzungumzaji wa kifasihi. Mlumbi hutumia lugha kwa njia inayovutia na kushawishi hadhira yake.

- Walumbi hutumia chuku kwa ufanifu mkubwa. Hata hivyo, lazima wadumishe adabu.

- Hutumia vipengele anuwai vya lugha kama vile sitiari, maswali ya balagha, methali, nahau ili kushawishi hadhira au kutilia mkazo wazo fulani.

- Katika baadhi ya jamii, walumbi walitumiwa kwa niaba ya viongozi kama vile machifu, wanaomba posa au kwa niaba ya ukoo.

- Hukuza ukakamavu wa kuzungumza hadharani. Mlumbi hupanda kuzunguza na hupenda kujisikia akizunguza mbele ya watu.

- Ulumbi hubainika katika miktadha ya kutoa hotuba au katika hali ambapo mtu anahitajika kutetea msimamo wake katika vikao.

(1 x 2)

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes